zungumze

Adabu wakati wa kula

Mwananchi Kimengele Kimode hapendi kulala usingizi. Atuletea tena mashauri yake kuhusu namna ya kuishi katika makundi ya watu.

wa siku za kisasa wa-
wengi huzoea kula me-
i pahali pa mkeka.
kula mezani lakini
kwa kulapo na adabu
uni zipo za kufwata.
vema mezani ukiwa
a na usilalie meza
bele wala usishikilie
havu kwa mikono yako.
sha kiwiliwili na
ono ya mbele uitue
ani. Usichezeshe mi-
chini ya meza na
chezecheze kitini
amoketi.
Chakula ukile na adabu
usiwe na haraka una-
jiandalia. Tumia kisu, uma na kijiko ginsi inavyoainishwa na desturi. Usikule kishenzi ama namna ya kimwitu. Haraka, haraka haina baraka. Saga kwa meno yako chakula na ukimeze kwa upole. Unapolula uimeze namna ya kimashamba na unapotafuna usifanye kelele kama vila mbwa.

Unapokunywa usigoromishe mlibo na usitonoe macho ukimtezama jirani wako wa mbele pa meza. Ukiisha kula na kunywa usibiole ukipahsa hivi wenzako kama umefurahiwa kula. Usinywe kama kinwa ni chenyi kujaa chakula. Husema lakini kama kwa waislam ni adabu kubiola ukishakula. Ukiwa mwungwana biola kwa nguvu zako zoté. Usipokuwaye, lakini, jikatalie.

Adabu mezani na msingi wa zingine zote ni kujua kama haupo peke na kama jirani yu mwenyi kuhitaji chakula na cha kunywa kama vile wewe. UKIJISAHAU KWA KUKUMBUKA JIRANI, UTAKUMBUKIWA NA JIRANI.

Kimengele Kimode.

JUA

Gazeti la Kivu

Mwaka wa 12 n° 286 **Tarehe 2 mpaka 8 Novemba 1985**

Kiongozi : Mutiri-wa-Bashara

amati kuu ya Chama

Kazi za mkusanyo wa kumi zimeanzishwa

Weregemere amepelekwa na pepo ya mapinduzi

Moja kwa moja kutoka
nshasa, mji mkuu wa
mhuri ya Zaïre, watu-
sha kuwa mnamo tarehe
Septemba iliyopita,
meanzishwa kazi za
utano wa 10 wa Kamati
u ya Chama chini ya
hunguzi wa raïs mwe-
ewe, muundaji wa Chama
etu cha Mapinduzi, Ma-
shali Mobutu Sese Se-
. Kazi hizo zitafanyi-
kisirisiri, mbali ya
pashaji wa habari, wa-
nga magazeti, wapiga
cha wa redio na tele-
sheni.

Kufuatana na habari hizo hizo inaaminika kuwa wanamemba wa kamati kuu ya Chama watachungua siasa ya ndani na ile ya nje ya Jamhuri nzima ya Zaïre. Siasa ya ndani ya nchi yetu itaelekea hasa matayarisho ya sherehe za kumbukumbu ya miaka 20 ya mapinduzi yetu, mambo inayoelekea masomo, uchumi wa nchi, vijana wa chama, afya na vivi hivi. Siasa ya nje ya Jamhuri ya Zaïre yahusu hasa zaidi umuhimu wa kurudi kwa Jamhuri ya Zaïre katika Jumuhia ya Umoja wa nchi huru za Afrika (OUA). Mbele ya yote, raïs Mobutu Sese Seko aliwapasha wanamemba wa kamati kuu ya Chama hatua iliyochukuliwa na wanamemba wa kiungo cha kilele cha ukumbo huo kutokana na kufukuzwa kazini kwa mwanamemba Weregemere Bingwa na kuachishwa kazi muda wa miezi 6 kwa mwenzie Birere Mabano.

Kaboyi Habimana.

Butembo kwa zone ya Lubero

Husema kama Butembo
Posta ya Beni, lakini
kweli nilifika Bute-
o nikaona kama ni wi-
ya (sous région) kwa
endeleo yaliyo katika
i ule. Maana mji ume-
nuka kwa jinsi ya
hangao sana. Nyumba
kila mtindo zimeje-
wa. Kuna nyumba za ku-
ndia juu ya zingine
tages). Mji umepangwa
ma kwa misitari mizu-
, kila njia ina jina
ke, na maneno yote ya-
yopitika katika miji
kubwa yanafanyika huko
a.

Maombi kwa serikali: yafaa serikali isaidie watu wa Butembo kwa kuendelesha mji ule, na watu wa kule wenyi juhudi watazidi kutumika. Maana kuna mambo yanawashinda, nayo ni haya :

1. Butembo wanapashwa kusaidiwa kwa kutengeneza ule mto ulio kati ya mji, kusudi mfereji ule wa mto ujengwe sawa wa kwetu Bukavu ule wa Kauwa. Ukisha kujengwa, nyumba hazitaanguka tena kwa ajili ya udongo kuliwa na maji ya mto na kusababisha mmomonyoko wa ardhi.
2. Serikali iwakumbuke kuwaletea moto mzuri kusudi mji wote uangare. Zile mashini za matajiri hazitoshelee kwa kuleta nuru kwa mji wote. Kila mtu anaangazia mahali pake, ile haitoshi kwa mji kama ule.
3. Wapatiwe barabara yenyi kuwa na kabulimbo kwa kuonyesha kweli mji vizuri, ingawa haifike mbali, kupatikane "ville" na "cité".

Mwimbaji wa Injili: Tambi Eae Munaongo.

HABARI ZA POPOTE

Amitabh Bachchan "Deewar" ageuka mwana-siasa

Kufuatana na habari zilizotolewa na mwandishi wetu Lubunga Bya' Ombe toka Kinshasa, yasemekana kuwa Amitabh Bachchan, bingwa katika michezo ya sinema ajulikananae kwa jina la "Deewar" alichaguliwa hapo majuzi kama mteule (député) wa jimbo la UTTAR-PRADESH ncini India baada ya uchaguzi uliofanyika nchini humo kwa kujipatia Bunge lipya. Bwana Amitabh Bachchan "Deewar" akiungana na Bwana RAJIV GANDHI, mtoto wa Bibi Indira Gandhi

Amitabh Bachchan "Deewar"

(aliyeuwawa mnamo siku zilizopita), waziri mkuu kwa sasa na prezidenti wa Chama cha "Congress" walijinyakulia sauti nyingi na kuwa hivi wajumbe wa jimbo lao kwenyi Bunge la Taifa nchini India.

Bwana Bachchan "Deewar" alitumwa kwenyi mji wa ALLAHABAD ambako alipokelewa na (fanatiques, admirateurs) mashupavu wake kwa shangwe na vigelegele.

Habari zilizotolewa na Gazeti "National Herald" la India, la tarehe 4 mpaka 10 januari 1985, zaeleza kuwa watu wengi walijipanga kando kando ya barabara alipopita saa moja mbele. Ilifaa vikosi vya polisi kuwachunga mashabiki wake wakilalamika kwa furaha "Amitabh Zindabad", "asifiwe Amitabh".

Kulingana na habari za gazeti hilo, bingwa huyo alijulisha kuwa si kwa kutoka katika umaskini wala kutafuta mali ndio maana aliomba kuchaguliwa. "Bali, alisema, shujaa huyo, ukomo wangu ni ule wa kutumikia raïa, ni wa kutafuta majawabu kwa magumu yanayowasonga wananchi wenzangu. Kwanza usafirishaji wa maji mashambani na penginepo, pili kupinga umaskini, tatu kuwatolea matibabu na madawa kazaa na inne kuhusika na hali ya mabarabara kwa usafirishaji ya watu na bizaa yao".

Tutawajulisha wasomaji wetu ya kuwa Bwana Amitabh Bachchan alicha mchezo wa sinema baada ya kupata ajali (accident) ambamo angepata kifo. Kwani ni karibu mwaka moja sasa, wakati alipokuwa akifanya mchezo wa sinema, mtu moja aliyemsikilia wivu alimvunja shina ya mgongo (colonne vertébrale) kwa kusudi.
Na baada ya ajali hiyo, waziri mkuu wakati huo, Bibi Indira Gandhi, akamwita kufanya siasa.

Bisimwa L-B. Tserou

Shabunda

Mkoa wa Bakisi katoka magumuni

Baada ya masimulizi mihimu yaliyofanyika kati ya Mwami Mopipi Bitingo na viongozi wa shirika la utengenezaji wa mabarabara "Office des routes", yajulishwa kuwa ujumbe moja wa chumba kinachohusika na ustawi wa kazi za ujenzi wa mabarabara za shirika hilo utajielekeza katika mkoa wa Bakisi mtaani Shabunda katika siku za usoni.

Ukomo wa safari ya ujumbe huo mkoani humo ni wa kufanya uchunguzi wa hali ya mabarabara na vilalo pia kupiga hesabu ya feza na vyombo vinavyoweza kutumikishwa kwa kurudisha mabarabara na vilalo vya mkoa wa Bakisi katika hali nzuri kama hapo zamani. Uchunguzi huo utafanyika kupitia vipande vya mabarabara toka Bukavu - Burhale - Kigulube - Katchunga hadi Shabunda. Bila kusahau za Shabunda - Matili - Kalole-Bukavu pamoja na Lugungu-Mapimo-Kasese.

Bisimwa L.-B. Tserou.